

Mpango wa ruzuku za pembejeo za kilimo ni nini?

Pembejeo za Kilimo cha Mapinduzi ya Kijani hujumuisha aina za mbegu zilizoboreshwa, mbolea za chumvichumvi na viuatilifu. Pembejeo hizi ni lazima zinunuliwe – mara nyingi kutoka kwa wakala wa serikali, muuzaji pembejeo za kilimo au mgavi wa kibiashara.

Neno ‘ruzuku’ lina maana kuwa mtu atatoa kitu ili kusaidia wakulima waweze kununua pembejeo hizo. Huyo ‘mtu fulani’ kawaida ni wakala wa serikali au mgavi wa kibiashara, na hicho ‘kitu’ kawaida ni mkopo wa fedha au aina ya utaratibu wa mkopo.

‘Ruzuku’ inaonekana kama vile serikali au mgavi wa kibiashara anafanya kitu kizuri kwa wakulima, **LAKINI** wakulima lazima wawe waangalifu juu ya **madhara ya muda mrefu** ya mikopo yoyote au mpango wa mikopo. Haya kwa kawaida huwafanya wakulima kuingia kwenye mtego wa madeni ambayo hawataweza kuukwepa. Nini kitatokea ikiwa utashindwa kulipa mkopo?

